# USCRI JUA HAKI ZAKO

## Mwongozo kwa Wahamiaji

Bila kujali hali ya uhamiaji, batu bote mu inchi ya Marekani bako na haki zenye zinalindwa na kuhakikishwa na Katiba. Hii mwongozo imetayarishwa kwa kujulisha batu benye habako banainchi ba Marekani kuhusu haki zao za kisheria mu hali mbalimbali wakati banakutanana na maafisa wa sheria na maafisa wa uhamiaji.

Sheria za majimbo **fulani** zinaweza kutofautiana. Sheria tofauti zinatumika mu **vituo ya ukaguzi** na wakati ya kuingia Marekani kupitia fasi rasmi za kuingilia mu inchi, sawa vile ku mipaka na ku viwanja ya ndege.

**Hii maelezo imetolewa kwa malengo ya elimu na haipashwi kutumiwa ku nafasi ya msaada wa kisheria. Kama weye ao mutu mwenye unajua anahitaji msaada wa kisheria, tafazali wasiliana na mwanasheria.**

## KAMA AFISA WA KUTEKELEZA SHERIA AO AFISA WA UHAMIAJI ANAKUSIMAMISHA MU NJIA



- Kama mutu anajitambulisha kuwaafisa wa kutekeleza sheria, umwambiye akuonyeshe beji ao kitambulisho yake. Andika namba ya kitambulisho yake.
- Polisi ao maafisa wa uhamiajibanawezakukuuliza jina yako.
- Bakikuuliza maswaliingine, unaweza kuuliza, "Je, mumenifunga?" Bakisema hapana, uliza, "Je, niko huru kuenda?" Kama jibu ni ndiyo, unaweza enda kwa utulivu.
  - Bakisema umesimamishwa na hauruhusiwe kuenda, uko na haki ya kujua ni juu ya nini.
- Bakijaribu kukuuliza maswali tena, sema mara moya, "Ningelipenda nizungumuze na mwanasheria mbele ya kujibiya ku maswali yoyote." Pale, afisa anapashwa acha kukuuliza maswali.



- Uko na haki ya kubakiya kimya kila wakati. Kila kitu yenye utasema inaweza kutumiwa zidi yako.
- Usiongeye juu ya hali yako ya uhamiaji ao ya urahiya na polisi ao maafisa wa uhamiaji.
- Usiamini ata kitu moya yenye polisi ao maafisa wa uhamiaji banaweza kusema kwa kukusukuma uongeye.
- Kama afisa wa uhamiaji anakulomba umuonyeshe barua zako za uhamiaji, unapashwa zionyesha kama uko nazo palepale. Hauna haja ya kuonyesha barua zako za uhamiaji kwa polisi wa eneo yako ao wa jimbo.
- Usiitike kufanyiwa ukaguzi ya mwili, sakoshi ao byenye uko nabyo. Kama polisi ao afisa wa uhamiaji anauliza kama anaweza kukagua bitu yako, uko na haki ya kusema hapana.
  - Afisa akikukagua, anaruhusiwa tu kupapasa sehemu ya nje ya nguo zako. Afisa hawezi finya ao kugusa ndani ya mifuko yako isipokuwa kama anaamini amesikiya silaha kisha kukupapasa.
  - Sema, "Sikubali kufanyiwa ukaguzi," hata kama banaendelea kufanya ukaguzi.
- Usitoshe bitu mu mufuko yako kwa hiari, usitupe byenye uko nabyo, wala usitiye mikono yako karibu na kiuno yako wakati afisa anakukaribia.
- Maafisa wa uhamiaji na polisi fulani wa majimbo banaweza kukuuliza jina yako, anuani yako na miaka yako, ao kukulomba kitambulisho yenye iko ako picha yako. Ukiulizwa, pana zile habari kwa utulivu na usiseme bongo.